

MOSHI CO-OPERATIVE UNIVERSITY (MoCU) CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI



MAHAFALI YA TATU YA CHUO KIKUU CHA USHIRIKA MOSHI (MoCU)

Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) anawatangazia wahitimu na wananchi wote kuwa Mahafali ya **TATU (3)** ya Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi yatafanyika siku ya **Ijumaa, tarehe 08 Disemba, 2017** kuanzia saa 4:00 asubuhi kwenye Uwanja wa Michezo wa Ushirika. Mkuu wa Chuo Mhe. Pius Msekwa atatunuku Astashahada, Stashahada na Shahada kwa wahitimu.

Wahitimu wote watakaohudhuria sherehe za mahafali hayo wanatakiwa kuthibitisha kwa **maandishi**, kupitia kwa Naibu Makamu Mkuu wa Chuo (Taaluma) S.L.P. 474, MOSHI, Barua Pepe: dvca@mocu.ac.tz kabla ya **Ijumaa, tarehe 24 Novemba, 2017**.

Kila mhitimu atakayeshiriki atazimishwa joho kwa gharama ya shilingi elfu thelathini tu (30,000/=). Joho litapatikana Chuoni siku ya **Jumatano, tarehe 06 Disemba, 2017** na **Alhamisi tarehe 07 Disemba, 2017** kuanzia saa 3:00 asubuhi mpaka saa 9:30 alasiri. Mwisho wa kurudisha majoho ni siku ya **Jumanne, tarehe 12, Disemba 2017** saa 9:30 alasiri. Faini ya shilingi elfu tano (5,000/=) itatozwa kwa kila siku itakayozidi. Malipo yafanyike kupitia MoCU Savings akaunti namba **01J2036991800** benki ya CRDB.

Mazoezi (rehearsal) kwa wahitimu yatafanyika katika Uwanja wa Michezo wa Ushirika **tarehe 07 Disemba, 2017** saa 8:00 mchana. Ambaye hatashiriki mazoezi hayo hatahudhurishwa. Cheti cha kuhitimu kitapatikana mara baada ya mahafali.

Sherehe ya kutunuku tuzo (Prize Awarding Ceremony) itafanyika siku ya **Alhamisi, tarehe 07 Disemba, 2017** kwenye Ukumbi wa J. K. Nyerere kuanzia saa 3:00 asubuhi.

**WOTE MNAKARIBISHWA
IMETOLEWA NA OFISI YA MAKAMU MKUU WA CHUO**



Vision: To become a Centre of Excellence in Co-operative Education and Practice



Centre of Excellence in Co-operative and Business Management Training of the East Africa Community (EAC)